

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI



## SHUKRANI KWA MHESHIMIWA RAIS KUPANDISHA MISHAHARA YA WATUMISHI WA UMMA KWA ASILIMIA 23.3

Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu, Utafiti, Sayansi, Teknolojia, Habari na Ufundi Stadi (RAAWU), kimepokea kwa furaha kubwa na shukrani nyingi uamuzi wa Mheshimiwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Mama Samia Suluhu Hassani kuongeza mishahara ya watumishi wa umma kwa kiwango cha asilimia ishirini na tatu nukta tatu (23.3%).

Uamuzi huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi kwani utachochea ari ya utendaji kazi kwa watumishi wa umma na tija itaongezeka Zaidi.

Uamuzi huu unaonyesha nia ya dhati aliyonayo Mheshimiwa Rais kwa maendeleo ya nchi na wafanyakazi kwani uamuzi huu umetanguliwa na matukio/maamuzi kadhaa ambayo ameyafanya kuhusiana na watumishi wa umma ambayo ni:

1. Kuruhusu upandishwaji wa madaraja kwa watumishi wa umma ambao ulisimama muda mrefu. Katika zoezi hili Mheshimiwa Rais amewapandisha madaraja watumishi **190,781** na kiasi cha Tshs. **39,649,988,204/=** zilitumika kuwalipa watumishi katika upandaji huo wa madaraja na vyeo.

2. Amelipa malimbikizo ya mishahara na madai mbalimbali ya watumishi wa umma takribani kiasi cha shilingi bilioni tisini na moja nukta **tisa (91.9 bilioni)**.
3. Ameruhusu wafanyakazi **19,386** wamebadilishwa kada na kulipwa kiasi cha Tshs. Bilioni moja, milioni mia tatu thelasini, laki tatu na elfu sita mia tano sabini na mbili **(1,330,306,572/=)**.

## **MISHAHARA KATIKA SEKTA BINAFSI.**

Ndugu waandishi wa Habari;

Pamoja na pongezi na shukrani zetu kwa Mheshimiwa Mamam Samia Suluhu Hassan kupandisha mishahara katika sekta ya umma, tunamuomba sana aiangalie pia sekta binafsi ambayo imeachwa pasipo kugushwa tangu ambapo waraka wa mwisho wa mishahara katika sekta binafsi ulitolewa mwaka 2013.

Kwa kuwa bodi ya kima cha chini cha mishahara katika sekta binafsi imekwishaundwa, tunaiomba serikali ihakikishe bodi hii pia itangaze mishahara katika sekta binafsi mapema iwezekanavyo.

RAAWU inawasihi wafanyakazi wote katika sekta ya umma na sekta binafsi kuongeza bidii katika utendaji kazi ili kuijengea uwezo serikali kutokana na tija itakayopatikana na kumdhihirishia Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kuwa nyongeza hii ya mishahara aliyotupatia watumishi wa umma imekuwa na faida pia kwa serikali

**JANE MIHANJI**  
MWENYEKITI WA RAAWU TAIFA  
16/5/2022